


# Mwongozo wa haraka kuhusu chanjo ya virusi vya korona

Maelezo mafupi kutoka kwa Taasisi ya Afya ya Umma ya Norwe (Norwegian Institute of Public Health) kuhusu chanjo ya kuzuia kuambukizwa COVID-19 (virusi vya korona).

---




## Kuhusu chanjo ya virusi vya korona

Chanjo hii itatolewa ka kila mtu anayependekewa kupokea chanjo.

Chanjo hailipishwi.

Chanjo hii inawalinda watu dhidi ya COVID-19.

---




## Je, unapokea chanjo kwa njia gani?

Chanjo inatolewa kwa sindano inayodungwa kwenye mkono.

Baadhi ya chanjo zinatolewa kwa vipimo viwili, cha pili kikitolewa baada yawiki chache.

Kumbuka kusema ikiwa una mizio, unatumia dawa, iwapo wewe ni mgonjwa au umekuwa na COVID-19.

---



## Je, chanjo inasaidia kwa njia gani?

Watu wengi hulindwa dhidi ya maambukizi ya COVID-19 baada ya wiki 1 - 2 baada ya kupokea chanjo kamili.

Fuata ushauri wa kudhibiti maambukizi hata kama umechanjwa.




## Je, chanjo inafanya kazi vipi?

Chanjo huufunza mwili kutambua na kujilinda dhidi ya kuambukizwa virusi vya korona.

Chanjo huondolewa mwili kwa haraka.

Hata hivyo, mwili hukumbuka jinsi ya kujilinda dhidi ya kuambukizwa virusi hivyo.




## Madhara ya chanjo

Chanjo imejaribiwa kwa kufanywa kwa tafiti kubwa kwa maelfu ya watu. Madhara ya kawaida ya chanjo ni:

- kuhisi uchungu mahali ulipodungwa sindano
- uchovu
- kuumwa na kichwa
- maumivu ya mwili
- kuongezeka kwa joto mwili au kuhisi baridi

Madhara haya yanakufanya usijihisi vizuri, lakini hutoweka baada siku chache.



## Madhara ya chanjo yasiyo ya kawaida

Wasiliana na daktari au mtaalamu mwingine wa afya ikiwa una dalili ambazo hazitarajiwi, kali au ambazo zinadumu kwa muda mrefu baada ya kupokea chanjo.